

For more information:

International Federation for Spina Bifida and Hydrocephalus: www.ifglobal.org

Association for Spina Bifida and Hydrocephalus (UK):
www.asbah.org


> *ASBAH Community*

> *Education Information*

Sheets

Enabling Education Network (EENET) : www.eenet.org.uk

Kitabu hiki kimeandaliwa na Shirikisho la Kimatafa la Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi pamoja na Norwegian Association for Spina Bifida and Hydrocephalus (RHF) | Michoro na Bert Dombrecht




Elimu mjumuiko “Karibu Shuleni”




Kitabu kwa ajili ya walimu,
watoto wa shule na wazazi wao

Mambo!




Ninakuja shuleni kwa mara ya kwanza nina furaha sana!
Nina shauku kubwa ya kuwa pamoja na mwalimu na watoto wengine wote.

Yaani nasubiri kwa hamu kuwa na na watoto wengine wote shuleni na michezoni!



Naweza kuhitaji **maelezo ya ziada** kutoka kwa mwalimu au mwenzangu ili nielewe.



Tafadhali fuatilia
kama nimeelewa vizuri kabisa.

Kama watoto wengine wote
Mimi ni mtoto wa
kipekee.

Pia nina hali inaitwa **Kichwa
Kikubwa na Mgongo Wazi.**

Nilizaliwa hivi hivi na daktari
anasema hali hii si kosa langu
wala la mama yangu.



Kichwa Kikubwa

Kichwa Kikubwa ni tatizo kwenye mshipa katika ubongo, litokealo mara kwa mara wakati wa kuzaliwa. Linaathiri mfumo wa fahamu (ubongo na mshipa ya fahamu). Hutokea katika mji wa mimba tumboni kwa mama katika wiki za awali za ujauzito wakati uti wa mgongo unaposhindwa kutengenezeka sawasawa. Hii husababisha kuharibika mfumo wa mawasiliano wa mshipa ya fahamu baina ya ubongo na sehemu nyingine za mwili.

Mgongo Wazi

Mgongo Wazi (pia huitwa “maji kwenye ubongo”) maana yake ni kuwa maji maji ya uti wa mgongo yamezidi kiwango cha kawaida kichwani kwa mtoto. Hali hii itahitaji kufanyika upasuaji au oparesheni. Mtoto mwenye hali hii huweza kupata matatizo ya uelewa na kujifunza kwa taabu.

Kuna matokeo tofauti ya jinsi gani mtoto mlemavu atakavyokua baadaye na athari ya ulemavu huu katika elimu.

Nina matarajio na ndoto kama watoto wengine na ninataka kujifunza kama watoto wengine wote. **Nikipewa msaada kidogo nitafanikisha mambo mengi.** Miguu yangu ni dhaifu **naweza kuhitaji msaada kuingia shule.**

Kukaa dawati la mbele karibu na mwalimu itanisaidia kusikia na kujifunza vyema.

Nahitaji **urahisi wa kwenda msalani.**

Kazi zangu za shule zitakuwa bora zaidi **kama nitapewa mapumziko** mara kwa mara.